

TANGAZO LA SERIKALI NA. 524 la tarehe 26/8/2022

SHERIA YA UMEME,

(SURA 131)

AMRI

(Imetolewa kwa mujibu wa kifungu Na. 23(2) and 24(2))

AMRI YA BEI YA UMEME (JUMEME RURAL POWER SUPPLY ("JUMEME")) YA MWAKA 2022

Jina la Amri

1. Amri hii itajulikana kama, Amri ya Bei ya Umeme (Jumeme Rural Power Supply ("Jumeme")), ya Mwaka 2022.

Bei zilizoidhinishwa

2. Bei za Umeme za Jumeme zilizoidhinishwa ni kama zinavyoonekana katika Jedwali la Amri hii.

Masharti

3. Bei zilizoidhinishwa zitaambatana na masharti kuwa:

- (a) Ifikapo tarehe 31 Desemba 2022 au kabla, Jumeme itawasilisha EWURA Mpango wa Kibiashara uliopitiwa upya kwa kuzingatia bei zilizoidhinishwa;
- (b) Ifikapo tarehe 30 Juni 2023, Jumeme watatakiwa kuwa wameboresha huduma ya umeme (kuondoa ukatikaji wa umeme) kwa wateja wake.
- (c) Jumeme itaendelea kuwasilisha EWURA taarifa zake za kifedha na kiutendaji kwa mujibu wa matakwa ya EWURA;
- (d) Ifikapo tarehe 31 Januari 2023 itawasilisha Mkataba wa Huduma Bora kwa wateja kwa ajili ya kupitiwa na kuidhinishwa.

JEDWALI

(limetengenezwa chini ya aya ya 2)

BEI ZILIZOIDHINISHWA

Kundi la Wateja	Wakati	Bei Iliyooombwa	Bei Zilizoidhinishwa (TZS/kWh)		
			2022	2023	2024
Majumbani	Mchana	5,226	1,470	1,690	1,710
	Usiku	5,226	1,470	1,690	1,710
Biashara	Mchana	3,902	1,340	1,540	1,560
	Usiku	5,853	1,440	1,650	1,670
Wazalishaji	Mchana	2,199	1,130	1,300	1,310
	Usiku	4,139	1,350	1,550	1,570

Dodoma
19 Agosti 2022

MODESTUS M. LUMATO
Mkurugenzi Mkuu